

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CHB.142/505/6

Tarehe: 15 Machi, 2024

**Yah: TANGAZO LA KUAHIRISHA USAHILI WA MAAFISA TEHAMA II
NA MAAFISA TEHAMA WASAIDIZI**

Husika na mada tajwa hapo juu na rejea tangazo la tarehe **04 Machi, 2024**.

2. Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inapenda kuwajulisha wasahiliwa wa Kada ya **Afisa TEHAMA Daraja la II** na **Afisa TEHAMA Wasaidizi** kuwa usahili uliopangwa kufanyika tarehe **16 Machi, 2024** umeahirishwa hadi tarehe **23 Machi, 2024** saa **2:00** asubuhi katika eneo la **Shule ya Sekondari Turiani**.
3. Hivyo wasahiliwa wenye ubobezi katika maeneo yaliyoainishwa hapa chini wanakaribishwa, maeneo hayo ni;
 - i. Mobile Application Developers
 - ii. Programmers
 - iii. Network
 - iv. Security
4. Aidha, wasahiliwa siku ya usahili wanatakiwa kuja na:-
 - i. Cheti cha Kidato cha Nne
 - ii. Vyeti vya Ujuzi (Professional)
 - iii. Cheti cha Kuzaliwa
 - iv. Kitambulisho cha Uraia/Mpiga Kura

Charles P. Lawisso
KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA